



Chotta Chama mtamu!

fikrapevu

@fikrapevu

@fikrapevu

BUSATI

Ukweli na Uhakika

Tovuti www.busati.mali.co.tz/ISSN 3456-3421 Na. 39, Jumatano Machi 5, 2025 Bei Tsh. 1000/= Ksh 100

Tanga yakubali maono ya Dk. Samia

Katika ziara yake mkoani humo, Rais Dkt. Samia ameeleza dhamira yake ya kuhakikisha Mkoa wa Tanga unakuwa pia mkoa wa utalii na kuwa....

- YAAHIDI KUHAKIKISHA MKOA HUO UNAZIDI KUPIGA HATUA
- TANGA INA HISTORIA KUBWA KATIKA MAENDELEO YA VIWANDA
- WANA TANGA WAPEWA SHUKRANI KWA UKARIMU WAO KWA RAIS

“ Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batilda Burian, amesema wataendelea kutekeleza maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha maendeleo ya mkoa huo yanaimarika, hususani katika kufufua viwanda na kuboresha miundombinu ya barabara.



Utafiti wa madini washika kasi

UJANGILI SASA WADHIBITIWA | USIYOYAJUA KUHUSU TWIGA

Tanga yakubali maono ya Dk. Samia

NA MWANDISHI WETU

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batilda Burian, amesema wataendelea kutekeleza maono ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha maendeleo ya mkoa huo yanaimarika, hususani katika kufufua viwanda na kuboresha miundombinu ya barabara.

Akizungumza mara baada ya ziara ya Rais Dkt. Samia mkoani humo, Balozi Dkt. Batilda amewashukuru wakazi wa Tanga kwa mapokezi mazuri waliyompata kiongozi huyo wa nchi na kuahidi wataendelea kusimamia kikamilifu fedha za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha zinaleta manufaa kwa wananchi.

“Tutaendelea kuimarisha maendeleo ya Mkoa wa Tanga kwa kuhakikisha rasilimali zinazotolewa na serikali zinatumiwa ipasavyo. Tanga ina historia kubwa ya viwanda, na jitihada za serikali ni kuirejesha katika nafasi yake kama kitovu cha viwanda nchini,” alisema Dkt. Batilda.

Aliongeza kuwa serikali imejipanga kuboresha mitandao ya barabara ili

kuwezesha urahisi wa usafirishaji wa bidhaa na kuinua uchumi wa mkoa huo. Wananchi wametakiwa kuunga mkono juhudi hizo kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na serikali.

Katika ziara yake mkoani humo, Rais Dkt. Samia ameeleza dhamira yake ya kuhakikisha Mkoa wa Tanga unakuwa pia mkoa wa utalii na kuwa unanufaika zaidi na fursa zitokanazo na fukwe, historia na tamaduni mbalimbali ndani ya mkoa huo.

Akizungumzia ziara yake ya wiki moja katika Mkoa wa Tanga, Rais Dkt. Samia alitoa rai kwa wananchi kutumia ipasavyo fursa za maendeleo zitokanazo na miradi mbalimbali na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ndani ya Mkoa wa Tanga.

Aidha, ametoa rai kwa wananchi kuhakikisha vijana wanapata ujuzi na stadi stahiki ikiwemo kupitia shule, vyo vya VETA vilijoyengwa katika kila wilaya, Chuo cha Mafunzo ya Amali cha Mkoa na kampasi ya Chuo Kikuu Mzumbe kinachotarajiwa kujengwa katika Wilaya ya Mkinga, ili waweze kunufaika zaidi na miradi mbalimbali inayofanyika katika mkoa huo.

Pindi Chana: Tumedhibiti ujangili

NA MWANDISHI WETU, Dodoma

WAZIRI wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameeleza kuwa wizara imeweza kudhibiti shughuli za ujangili katika maeneo yaliyohifadhiwa na kupelekea ongezeko la idadi ya wanyamapori ikiwemo Tembo, Simba, Chui na Nyati.

Balozi Dkt. Chana ameyasema hayo katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani, yaliyofanyika katika Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma juzi, ambapo alipongeza taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuendelea kusimamia maeneo yaliyo hifadhiwa na kupambana na ujangili.

“Nchi yetu inaongoza kwa idadi kubwa ya wanyamapori, tunayo idadi kubwa ya Simba, Chui, Nyati na niseme kwamba Tanzania ni ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya Tembo Duniani,” aliongeza Balozi Dkt. Chana.

Naye, Mkurugenzi wa Wanyamapori

Tanzania, Dkt. Allex Lobora alieleza umuhimu wa kuadhimisha siku hiyo ambapo inaikumbusha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili zetu ikiwemo wanyamapori na mimea iliyo hatarini kutoweka, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia ujangili.

Dkt. Lobora aliongeza “Siku hii inatoa fursa ya kuonyesha mchango wa wanyamapori katika maisha ya binadamu pamoja na kuhamasisha hatua za kulinda wanyamapori kwa manufaa ya vizazi vijavyo”

Aidha, kaulimbiu ya maadhimisho hayo inasema “Wanyamapori na Uwekezaji Kifedha, Wekeza kwa Watu na Dunia” huku ikihimiza kuwa na mifumo na mikakati endelevu ya kupata na kusimamia matumizi ya rasilimali ili kufikia lengo la uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori.

Maadhimisho hayo yalitanguliwa na maandamano ya amani kutoka Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii Swagaswaga kuelekea Viwanja vya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma ambapo Balozi Dkt. Chana alitembelea mabanda yaliyokuwa yakitoa taarifa kuhusu elimu uhifadhi na utalii.

Utafiti wa madini washika kasi

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa amekutana na Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Chen Mingjian katika kikao kilicholenga kujadili fursa na maeneo mbalimbali ya ushirikiano katika Sekta ya Madini ikiwa ni mwendelezo wa mazungumzo kati ya Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango na kiongozi huyo .

Katika mazungumzo yao, Dkt. Mpango aliiomba Serikali ya China kupitia balozi huyo kusaidia shughuli za utafiti wa madini Tanzania, ambapo baada ya mazungumzo yao, Serikali ya China imetuma wataalam wawili kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti ya nchini humo ili kufuatilia na kujua mahitaji ya utafiti na maeneo mengine ya mashirikiano kati ya Tanzania na China

“Kikao nilichokiongoza kimejadili maeneo ya ushirikiano na sisi kwa upande wetu tumeweza kubaini maeneo matatu muhimu ambayo Serikali ya china inaweza kutusaidia katika shughuli za utafiti na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara kulingana na mahitaji,” amesema Dkt. Kiruswa.

Maeneo matatu ambayo wataalam wa wizara wakiongozwa na Dkt. Kiruswa waliyoweza kuyabaini ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia (high resolution airborne geophysical survey) hususani kwa kuanzia eneo la Mkoa wa Dodoma;

Maeneo mengine ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa fursa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika maeneo ya teknolojia za kisasa kama vile ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za jiosayansi; na kusaidia kuleta teknolojia za kisasa za utafiti na uchakataji wa taarifa za utafiti wa madini ikiwa ni pamoja na matumizi ya ndege nyuki katika utafiti wa madini nchini.

Majaliwa: Sekta ya kifedha kupiganiwa

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Amesema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Amesema hayo juzi alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya

kuboresha huduma jumuishi za kifedha.

“Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 - 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022”

Majaliwa alisema kuwa, jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034.

“Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali.”

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemu amesema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuatake viwango bora vya usalama wa mitandao na kugundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. “Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi.”

Pia, Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha wananchi wengi wana namba za NIDA ambazo zinarahisisha ufanyaji wa biashara, utambuzi wa mtu na hivyo kumuwezesha kufungua akaunti.

TAMISEMI yajipinga Bima ya Afya

NA MWANDISHI WETU

MKURUGENZI wa Idara ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Rashid Mfaume, amesema kuwa katika kuelekea utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, TAMISEMI imejipanga vyema kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora huduma za afya katika ngazi ya msingi.

Dkt. Mfaume ametoa kauli hiyo alipokuwa katika ziara yake ya kukagua utoaji wa huduma za afya, lishe, na ustawi wa jamii mkoani Dodoma, ambapo alitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kondo.

Amesema TAMISEMI itahakikisha katika ngazi ya afya ya msingi bidhaa

zote muhimu za afya zinapatikana.

“Tunawahakikishia Watanzania kuwa katika ngazi ya huduma za afya ya msingi, Ofisi ya Rais TAMISEMI imejipanga kuhakikisha wananchi wote wanaojiunga na Bima ya Afya kwa Wote wanapata huduma zote stahiki kama inavyotakiwa,” amesema Dkt. Mfaume.

Aidha, amebainisha kuwa hapo awali kulikuwapo na changamoto ya baadhi ya wanachama wa bima ya afya kukosa dawa katika vituo vya kutolea huduma na kulazimika kununua dawa hizo wenyewe.

Hata hivyo, kwa sasa TAMISEMI imechukua hatua kuhakikisha vituo vya afya vinakuwa na akiba ya kutosha ya dawa na vifaa tiba ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Elimu ya mikopo yatolewa

NA ALBANO MIDELO, Songea

WANA vikundi vya wajasiriamali na wafanyabiashara waliokidhi vigezo vya kupata mkopo wa asilimia kumi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wamepatiwa mafunzo ya mwisho kabla ya kupokea mikopo hiyo.

Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Klasta Mlingoti, mjini Tunduru yakiwa na lengo la kuwaandaa wanufaika kwa matumizi sahihi ya mikopo ili kukuza biashara zao.

Mada zilizofundishwa zilihusisha usimamizi wa fedha, uandishi wa mipango ya biashara, mbinu mbalimbali za kibiashara, na umuhimu wa kurejesha mikopo kwa wakati.

Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii katika halmashauri hiyo, Jeceline Mganga, aliwasisitiza wanufaika kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili waweze kupata faida na kurejesha mikopo bila usumbufu.

“Unaporejesha kwa wakati, unajiongezea sifa ya kukopa zaidi, mikopo ii haina riba, hivyo ni fursa ya kipekee kwa wajasiriamali kuhakikisha inawanufaisha,” alisema Jakline

Unataka kufanya biashara ya utalii?

UKIANZA biashara yoyote changamoto za mwanzoni ni nyingi sana na ni muhimu kufahamu changamoto za biashara ndogo ndogo.

1. Maumivu

Kila mtu aliyefanikiwa amepitia kwenye safari yenye maumivu na ikumbukwe kuwa kupita njia yenye changamoto ndiko hutuelekeza kwenye mafanikio.

Jifunze kutumia changamoto na maumivu kuwa kama hamasa ya kufanya juhudi zaidi kufikia mafanikio.

Hakuna haja ya kulalamika na kukata tamaa bali anzia ulipo kwenda mbele ili kukamilisha malengo yako.

2. Kukata Tamaa

Wengi waanzapo safari ya mafanikio huanza kwa kasi kubwa kwani wao hufikiri tu juu ya mafanikio.

Lakini katika ukweli halisi ni kuwa, mwanzoni kuna changamoto lukuki ambazo usipotazama malengo yako ni rahisi kukata tamaa.

Kipindi hiki kimekuwa kigumu sana kwa watu wengi kwani hawaoni ile nuru ya awali tena bali wanaona changamoto kila kukikucha.

Kumbuka wahenga walisema “mwanzo ni mgumu”; jitahidi usirudi nyuma nawe utaona matokeo yake.

Mambo ya kufanya kama unataka kukata tamaa: Uliza waliokutangulia walifanyaje kutatua hizo changamoto unazoziona. Soma vitabu na makala mbalimbali za kukuhamasisha. Jikumbushe juu ya malengo yako na matokeo utakayoyapata utakapokuwa umevuka kwenye hizo changamoto.

3. Utapoteza Mahusiano

Katika safari ya kuelekea kufanikiwa mambo mengi hutokea, kama vile kupoteza fedha, vitu, na watu.

Kumbuka kuwa siyo watu

wote watakaoweza kwenda pamoja na wewe katika safari hii, kwani kuna wengine hawana hamasa uliyo nayo, hawapendi ufanikiwe, wana mambo au shughuli zao.

Hivyo usishangae hata watu wa karibu uliokuwa unawategemea wakakuacha bila msaada wowote au wakabadilika sana.

Jipe moyo, fanya bidii tambua mnufaika wa kwanza wa mafanikio yako ni wewe wala sio wao.

4. Utakatishwa Tamaa

Katika njia ya mafanikio kuna watu wachache sana wenye mawazo chanya na wanaopenda mafanikio yako.

Hivyo basi, utakutana na watu wengi sana watakao kukatisha tamaa na kukutisha ili urudi nyuma.

Utawasikia wakisema hili hautafanikiwa, hili halikufai, fulani alifanya akashindwa au halinipi faida.

Jambo la kufanya hapa ni kulinda fikra na nafsi yako visipokee mawazo na misimamo ya hawa watu kwani kwa kufanya hivi utaweza kutazama tu lengo lako na kufanya bidii kulifikia.

5. Utachukiwa



Kwa hakika binadamu hapendi mafanikio ya mwingine, moyo wake hujaa chuki, maumivu na husuda pale mwingine anapofanikiwa.

Wapo watu wanaotamani ubaki kama ulivyo na usiweze kufanya kitu cha kuwazidi wao au walichoshindwa kukifanya.

Nimeshuhudia marafiki zangu kadhaa wakipunguza uhusiano na mimi pale waliponiona nimepata mafanikio kadhaa hasa kuwazidi wao.

Hivyo basi, badala ya kupambana na wenye wivu na chuki pambana na malengo yako, kisha mafanikio yako yatawapa somo.

6. Utajilaumu Mwenyewe

Kujilaumu hakuepukiki katika safari ya mafanikio hasa pale unapokuwa umepata tatizo au hasara kwa uamuzi uliufanya hapo awali.

Kwa hakika, huwezi kubadili uamuzi au tendo lililopita badili uelekeo wa maisha yako ya baadaye kuanzia ulipo.

Usijilaumu tena kwani utauwa ile hamasa yako ya ndani na hutoweza kufikia mafanikio yako.

Mabadiliko ya Tabia Nchi: Mambo 5 ya kuzingatia mwaka huu

JMJI wa Amazon wa Belem, Brazili, utakuwa kitovu cha juhudi za kimataifa za kukabiliana na janga la mabadiliko ya tabianchi mwezi Novemba 2025, wakati utakapoandaa moja ya mikutano muhimu ya Umoja wa Mataifa ya mabadiliko ya tabianchi hivi karibuni.

Hadi wakati huo, kutakuwa na fursa nyingi za kufanya maendeleo makubwa katika masuala kadhaa yanayohusiana na tabianchi, kuanzia kwenye viwango vya kushangaza vya uchafuzi wa plastiki hadi kufadhili mpito wa kuhamia uchumi wa kimataifa unaojali mazingira.

1. Je, tunaweza kuhakikisha lengo la nyuzi joto 1.5 linakuwa hai?

“Kuhakikisha lengo la nyuzijoto 1.5 linakuwa hai” imekuwa kilio cha hadhara cha Umoja wa Mataifa kwa miaka kadhaa, ikimaanisha lengo la kuhakikisha kuwa wastani wa joto duniani hauzidi nyuzi joto 1.5 zaidi ya viwango vya kabla ya mapinduzi ya viwanda.

Makubaliano ya kisayansi ni kwamba kutochukua hatua kutakuwa na matokeo ya janga, haswa kwa mataifa yanayoitwa ‘mstari wa mbele’, kama vile mataifa yanayoendelea ya visiwa ambayo yanaweza kutoweka chini ya bahari huku viwango vya bahari vikiongezeka.

Katika COP30, mkutano wa mabadiliko ya tabianchi wa Umoja wa Mataifa uliopangwa kufanyika kuanzia tarehe 10 hadi 21 Novemba 2025, upunguzaji yaani, hatua na sera za kupunguza utoaji wa gesi chafuzi zinazochangia kuongezeka kwa joto unatarajiwa kuwa lengo kuu.

Mataifa kote duniani yatawasili yakiwa na ahadi dhabiti na zenye malengo makubwa zaidi ya kupunguza gesi joto. Hii yote ni utambuzi kwamba ahadi zilizopo hazitoshelezi kabisa kukabili viwango vya joto, na ni sehemu ya makubaliano ambayo nchi wanachama zilitia sainsi mwaka wa 2015 katika Mkataba wa Paris wa mabadiliko ya tabianchi COP, mataifa yanapaswa “kuongeza ahadi zao kila baada ya miaka mitano.

Mara ya mwisho hii ilifanyika ilikuwa ni mjini Glasgow kwenye mkutano wa COP mwaka 2021, ambayo ilicheleweshwa kwa mwaka mzima kutokana na janga la COVID-19.

2. Kulinda asili

Kufanya COP30 katika eneo la msitu wa mvua wa Amazon huko Brazili ni muhimu sana. Inakumbusha juhudi za kwanza za kimataifa za kulinda mazingira: “Mkutano wa Dunia”, ambao ulisababisha maendeleo ya kuwepo mikataba mitatu ya mazingira juu ya mabadiliko yatabianchi, bayoanuwai na kuenea kwa jangwa, ulifanyika katika jiji la Brazil la Rio de Janeiro mwaka 1992.

Eneo hilo la msitu wa mvua pia linaonyesha jukumu ambalo

asili inachukua katika janga la tabianchi. Msitu wa mvua ni “beseni kubwa la hewa ukaa,” mfumo ambao unachukua na kuhifadhi gesi chafuzi ya ukaa au CO2 na kuizuia kuingia kwenye angahewa, ambako inachangia ongezeko la joto duniani.

Kwa bahati mbaya, misitu ya mvua na “suluhu zingine za asili” ziko chini ya tishio kubwa kutoka kwenye maendeleo ya binadamu, kama vile ukataji miti haramu ambao umeharibu maeneo makubwa ya eneo hilo.

Umoja wa Mataifa utaendelea na juhudi zake za kuboresha ulinzi wa misitu ya mvua na mifumo mingine ya ikolojia mwaka 2024, wakati mazungumzo ya bayoanuwai yatakapoanza tena mjini Roma mwezi Februari.

3. Nani atalipia gharama?

Fedha kwa muda mrefu imekuwa suala mwiba katika mazungumzo ya kimataifa ya tabianchi. Nchi zinazoendelea zinahoji kuwa nchi tajiri zinapaswa kuchangia zaidi katika miradi na mipango ambayo itawawezesha kuondokana na nishati ya mafuta kisukuku na kuimarisha uchumi wao kwa vyanzo vya nishati safi.



Hawa ndo' wakali wao mbugani

LEO ngoja tujifunze kuhusu wanyama wakubwa watano barani Afrika ambao ni Simba, Tembo, Faru, Chui kwanini waitwe hivyo, tabia zao na hata wanakopatikana kwa wingi barani Afrika, bila kusahau hali au ngazi ya uhifadhi wao, karibu.

Makala hii imeainisha wanyama watano ambao ndio mabingwa katika mbuga za Afrika, jina hili walipewa miaka ya nyuma na wawindaji wa kampuni za uwindaji kutokana na kuwa ni vigumu sana na hatari zaidi kuwawinda, bado jina hili linatumika kwa sasa japokuwa ni kwa makampuni ya utalii mbugani kwani ni fahari kwa mtalii kukutana nao mbugani katika mazingira yao na pia kupata fursa ya kipekee kupiga nao picha.

Ni furaha iliyoje kukutana na Simba akiwa mawindoni pembeni jua linazama? Haielezeki, vipi tabasamu usoni unapokutana na Chui uso kwa uso macho kwa macho. Tembo je? Mnyama mkubwa nchi kavu duniani na mwenye uwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu na hisia kama binadamu?

Au Kifaru mnyama alae majani wakati wa usiku tofauti na wala majani wengine? Inakuwaje tena kukutana na Nyati jamii pekee ya ng'ombe aishie mbugani na asiyehofia chochote?

Basi mpendwa msomaji wetu hao ndio mabingwa au nyota tano mbuga za Afrika japokuwa wengine hawana umbo kubwa kama ulivotegemea, makala imechambua mmoja baada ya mwingine.

Simba

Ndiye mnyama pekee miongoni mwa walao nyama ambaye hana adui mbugani zaidi ya binadamu, magonjwa na uharibifu wa mazingira,



la Sahara; na 10% waliobaki duniani hupatikana hifadhi ya taifa Ruaha-Tanzania

Simba ndiye mfalme wa mbuga kutokana na sifa kuu tano za kipekee alizonazo japo leo nitataja tatu

Muungurumo anaotoa Simba dume, ile sauti inaweza

pia kwa kiikolojia anashika nafasi ya juu zaidi katika ngazi ya ulaji chakula katika mfumo wa viumbe hai (Africans' apex predators) na pia anashika nafasi ya pili kwa umbo kubwa katika jamii za paka duniani.

Pia simba ndio paka pekee wanaoishi katika makundi makundi (pride) kuanzia watatu mpaka thelathini (3-30) kwa sababu wanahitajiana zaidi, hata hivyo jike pekee ndio wanaoishi kutegemea makundi hayo mpaka kifo hii ni kutokana na kwamba wanasaidiana kutunza watoto ndani ya kundi kwa pamoja pia watoto hao hunyoya kwa Simba jike yoyote anayetoa maziwa.

Chakula; nyama, haswa ya wanyama wakubwa wenye kwato mfano jamii ya Swala, Nyati

Usichokijua

Simba jike ndiye huwinda mara nyingi hasa wakati wa usiku wakiwa kwenye kundi na mara nyingine kuiba au kunyang'anya mnyama aliyetoka kuwindwa na wanyama wengine kama fisi, pia ndiye mlinzi wa makazi yao.

Jamii ya paka pekee wanaoishi kwenye makundi tofauti na wengine kama chui na chui milia ambao mara nyingi wanakaa peke yao kipweke zaidi.

Simba waliopo barani Afrika wanapatikana asilimia 8% tu ya maeneo tengefu ya hifadhi za wanyamapori zilizopo Afrika na wengi wao wanaoishi mbugani hupatikana kusini mwa jangwa

kusikika maili tano kutoka sehemu alipo na hivyo kurahisisha mawasiliano na walio mbali na pia njia moja wapo ya kulinda himaya yake.

Anashika nafasi ya kwanza kwa wanyama jasiri zaidi duniani, hivyo hatishiwi na kitu chochote.

Ndevu nyingi na ndefu alizonazo Simba dume zinazoanzia kidevuni hadi shingo inapoishia humfanya awe na muonekano wa kipekee miongoni mwa wanyama wa porini.

Pia Simba huwasiliana kwa kugusanisha vichwa vyao na hapo hubadilishana harufu iliyobeba habari kuhusu shughuli aliyotoka kufanya Simba huyo, hali zao pia ni njia mojawapo ya kuimarisha mahusiano yao.

Chui

Chui ndiye Paka pekee barani Afrika wenye nguvu na uwezo mkubwa wa kupanda miti na mwenye uwezo mkubwa wa kuona usiku kuliko paka wengine hivyo humfanya kutokuonekana mara nyingi mbugani.

Chakula; nyama, saizi ya kati wanyama wenye kwato na wanyama wadogo wadogo

Usichokijua

Chui ni wanyama wapekwe hukaa peke yao muda mwingi isipokuwa hukutana wakati wa kujamiiana na kukuza chui watoto.

Ramadhani: Kile kinachotukia mwilini pale unapofunga

KILA mwaka mamilioni ya Waislamu duniani hufunga tangu jua linapochomoza mpaka linapotuwa kwa siku 30 mfululizo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Katika miaka ya hivi karibuni, Ramadhan hujiri katika miezi ya joto na katika maeneo ya kaskazini hilo mara nyingine humaanisha watu kufunga kwa saa nyingi na katika hali ya hewa yenye joto jingi.

Baadhi ya nchi kama Norway, waumini hufunga kwa hadi saa 20 kwa siku mwaka huu. Basi hili lina manufaa yoyote? Haya ndiyo yanayofanyika mwilini mwako unapofunga kwa siku 30.

Siku za kwanza

Kimsingi mwili wako hauingii katika hali ya kufunga mpaka saa nane au zaidi baada ya kula chakula chako cha mwisho. Huu ndio wakati utumbo unamaliza kusaga chakula na kunfyonza madini kutoka chakula ulichokila.

Muda mfupi baada ya hili, mwili wetu huanza kutafuta glucose iliopo kwenye maini na misuli kutafuta nguvu mwilini.

Muda unavyosogea, baada ya glucose iliopo mwilini kumalizika, miwili hugeukia mafuta kutafuta nguvu.

Mwili unapoanza kuchoma mafuta, hili husaidia kupunguza

uzito wa mwili, hupunguza viwango vya cholesterol na kupunguza hatari ya kuugua kisukari.

Hata hivyo kushuka kwa viwango vya sukari mwilini inasababisha mwili kudhoofika na kukosa nguvu. Huenda ukaanza kuumwana kichwa, ukasikia kisunzi, kichefuchefu na harufu mbaya kutoka mdomoni.

Kiwango cha njaa

Jihadhari na mwili kupungua maji- Siku ya 3-7

Mwili unapoanza kuzoea kufunga, mafuta yanayayuka na kugeuka sukari mwilini.

Ni lazima ujirudishie maji mwilini kufidia masaa uliokuwa umefunga, la sivyo unapotokwa na jasho unaweza kupungua maji mwilini.

Ni muhimu chakula chako kijukuisha 'lishe yenye kukupa nguvu', kama vile vyakula vyenye uwanga na vya mafuta kidogo. Ni muhimu kuwa na lishe bora, ikiwemo protini, chumvi na maji.

Siku ya 8-15

Katika awamu ya tatu, utaona hali inaimarika, kama vile hisia wakati mwili unaanza kuzoea kufunga.

Dkt. Razeen Mahroof, mshauri katika Hospitali ya Addenbrooke huko Cambridge, Uingereza anasema kuna manufaa mengine.

"Katika maisha yetu ya kawaida huwa tunakula vyakula vyenye kalori nyingi tu, na hili huweza kuuzuia mwili kutekeleza majukumu mengine kama kujirudisha katika hali yake ya kawaida.

"Hili husawazishwa wakati mtu anapofunga,

huruhusu mwili kuangazia kazi nyingine. Kwa hivyo kufunga huenda kukaunufaisha mwili kwa kuuponya na pia kuzuia na kupambana na maambukizi."

Siku ya 16 -30

Katika nusu ya mwisho ya Ramadhan, mwili wako utakuwa umeshazoea kabisa kufunga. Maini, figo na utumbo na ngozi yake zitakuwa zinajitakasa kufikia sasa.

"Kiafya, kufikia kiwango hichi viungo vyako ndani ya mwili vimerudi kufanya kazi kikamilifu, huenda kumbukumbu yako ikawa imeimarika na ukawa na nguvu zaidi," anasema Dkt Mahroof.

"Mwili wako hautafuti protini ya kuupa nguvu hili ni wakati uanapokuwa na 'njaa' na kutumia misuli kuupa nguvu. Hili hufanyika iwapo utafunga kwa muda mrefu mtawalia.

"Kwasbabau watu hufunga ramadhan tangu alfajiri mpaka jioni, kuna nafasi nzuri ya kurudisha nguvumwilini kutokana na vyakula na vinywaji. Hii huhifadhi misuli lakini pia husaidia katika kupunguza uzito mwilini."

Kufunga kuna manufaa?

Dkt. Mahroof anajibu ndio, lakini kwa sharti moja. "Kufunga kuna manufaa kwa afya yetu kwasababu inatusaidia kulenga tunachokula na wakati tunapokila. Hata hivyo japo kufunga kwa kipindi cha mwezi mmoja ikawa ni sawa, sio vizuri kufunga mfululizo baada ya Ramadhan.

"Kufunga mfululizo sio vizuri katika kutafuta kupunguza uzito wa mwili kwasababu hatimaye mwili utaacha kugeuza mafuta kuwa nguvu na badala yake utageukia misuli. Hili sio jambo zuri na ina maana mwili wako utaishia kudhoofika kwa njaa."

Anapendekeza kwamba kufunga kando na katika mwezi wa Ramadhani au kufunga kwa siku tano na kupumzika siku mbili ni vizuri kuliko kuamua kufunga kwa miezi kadhaa mfululizo.



TRUMP AIPA KIBANO UKRAINE

RAIS wa Marekani Donald Trump amesitisha misaada yote ya kijeshi kwa Ukraine kufuatia mzozo wake na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy wiki iliyopita, amesema afisa wa Ikulu ya White House.

“Rais Trump amekuwa wazi kuwa anataka amani. Tunataka pia washirika wetu wajitolee kwa lengo hilo. Tunasitisha misaada yetu na kuikagua ili kuhakikisha inachangia katika suluhu,” alisema afisa huyo, akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Ikulu ya White House haijaleza aina na kiasi cha misaada itakayositishwa au muda wa kusitisha utadumu kwa kipindi gani. Pentagon pia haijatoa maelezo zaidi.

Ofisi ya Zelenskiy haijatoa majibu kwa maswali ya Reuters kupitia Ubalozzi wa Ukraine huko Washington.

Hatua hiyo imekuja baada ya Trump kupindua sera za Marekani kuhusu Ukraine na Urusi alipoingia madarakani mwezi Januari, na kuchukua msimamo wa urafiki zaidi kwa Moscow.

Haya yanakuja baada ya mabishano makali kati ya Trump na Zelenskiy katika Ikulu ya White House siku ya Ijumaa ambapo Trump alimtuhumu kwa kutoshukuru vya kutosha kwa uungaji mkono wa Washington katika vita na Urusi.

Mara baada ya Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy kufukuzwa Ikulu ya Marekani kufuatia malumbano yake na Rais Donald Trump na Makamu wa Rais JD Vance, viongozi wa Ulaya walituma jumbe nyingi kumuhakikishia kwamba watasimama naye hadi dakika ya mwisho.

Siku iliyofuata tu ya Jumamosi iliyopita, Zelenskiy alitua

Uingereza, akaonana na Waziri Mkuu wa nchi hiyo Kier Starmer na hata kufanya mazungumzo na Mfalme Charles. Siku ya Jumapili aka kutana na viongozi wa Ulaya waliokutana London kujadili mustakabali wa usalama wa bara lao.

Pamoja na maonyesho yote haya, swali kubwa ni; Ulaya ina ubavu wa kuisaidia Ukraine kijeshi ikiwa Marekani itakaa pembeni?

Jibu la haraka ni; Hapana, haina uwezo huo katika uvamizi huu wa sasa wa Urusi.

Uhaba wa bajeti

Kuna vitu vingi Ulaya inahitaji kuweka sawa, muda ni mchache na haina utashi wa kisiasa wa kutosha.

Ukianza na bajeti ya kijeshi tu, kwa mujibu wa International Institute of Strategic Studies, bajeti ya kijeshi ya Urusi kama nchi ni kubwa kuliko ile ya bara zima la Ulaya. Wakati Urusi imetenga 6.7% ya pato lake la taifa, wakati Ulaya (wanachama wa Nato ukiondoa Marekani) wanatumia wastani wa 1.6%.

Ili kukabiliana na Urusi, wataalamu wanasema Ulaya



itapaswa kuongeza matumizi yake ya kijeshi hadi kufikia wastani wa 3.5% ya pato la taifa la umoja huo, hasa kwa nchi za Mashariki ya Ulaya zilizo karibu na Urusi kama vile.

Tayari tunaona nchi kadhaa za Ulaya zimeanza kuongeza bajeti yao ya kijeshi. Uingereza kwa mfano, siku chache zilipopita imetangaza mpango wa kukata pesa inayotuma kwa misaada nje ya nchi na kuelekeza katika bajeti yake ya ulinzi.

Uwanja wa mapambano

Kuhusu wanajeshi walio tayari kupigana, wakati Urusi ina wanajeshi takribani 250,000 walio tayari kupelekwa Ukraine

muda wowote, Ulaya haiwezi kutoa wanajeshi 150,000, ambao Zelenskiy anasema watahitajika kulinda amani na kumzuia Putin asivamie tena.

Viongozi wengi wa Ulaya wamesema wakijitahidi sana, basi wanaweza kupeleka wanajeshi wasiozidi elfu thelathini (30,000).

Ulaya inakabiliwa na ukosefu wa kiongozi mmoja (mtu au ofisi) wa kijeshi. Kwa ujumla Ulaya (wanachama wa Nato) ina wanajeshi wapatao 1.47 ambao wako tayari kupigana, lakini hawana komandi moja ya kuwakusanya na kuwaongoza. Kwasasa Nato inategemea hii kazi kufanywa na Marekani.

Hivyo Marekani akikaa pembeni, Ulaya itakuwa na kazi ya kutafuta kiongozi ambaye anaweza kuvikusanya, kuvijumuisha na kuviongoza vikosi vya nchi zote za Ulaya wanachama wa Nato kuwa kikosi kimoja chenye nguvu, badala ya kila nchi kwenda kukabiliana na Urusi kama nchi moja moja.

Ulaya ina teknolojia ya kutosha, lakini inahitaji uwekezaji mkubwa kuanza kutengeneza vifaa vikubwa na bora zaidi hasa vya masafa marefu kama ambavyo Marekani imetoa kwa Ukraine ndani ya miaka hii mitatu.

Silaha za anga na utashi wa kisiasa

Nchi za Ulaya pia zinategemea vifaa vya anga vya

Marekani na uwezo wake mkubwa wa kukusanya intelijensia, uwezo ambao Ulaya haina.

Hata katika usafirishaji wa silaha, Ulaya imekuwa ikitegemea sana miundombinu na uratibu wa Marekani kufanikisha kusafirisha msaada wa vifaa uliopeleka Ukraine.

Wakati Nato inavamia Libya mwaka 2011, hata kama Ulaya ndio ilikuwa inaongoza mapambano, walitegemea zaidi vituo vya mafuta vya Marekani kujaza vifaa vyao.

Ulaya inahitaji kiongozi katika masuala ya dunia, kama ambavyo Marekani imekuwa.

Aidha Ujerumani au Ufaransa inaweza kuchukua nafasi hii, lakini nchi tatu; Ujerumani, Ufaransa na Uingereza zinahitaji kuwa katika ukurasa mmoja, zikazungumza lugha moja na zikawa na utayari wa pamoja kuongoza nchi zingine 27 za Nato katika kuikabili Urusi.

Mbali na uwezo wa kifedha na kijeshi, nchi nyingi za Ulaya zinakabiliwa na mikingamo na mivutano ya kisiasa ndani ya nchi zao, zingine zikiwa na idadi kubwa ya wananchi wasiotaka nchi zao kujihusisha moja kwa moja na vita kwa ujumla na hasa mapigano na nchi kubwa kama Urusi.

Utayari wa serikali nyingi za Ulaya kuingia vitani na Urusi kutategemea utashi wa kisiasa na wananchi kwa ujumla kutoka nchini mwao, jambo ambalo ni changamoto kwa nchi nyingi za Ulaya.

Hizi ni baadhi ya sababu zinazowafanya nchi nyingi za Ulaya kuendelea kuiangukia Marekani itoe hakikisho la ushiriki wake katika kuisaidia Ukraine kupambana na Urusi na kulinda mkataba wa amani ili Urusi isiukiuke.

Kizungumkuti cha NATO

Tangu awamuyakwanza, Trump amekuwa akitishia kupunguza mchango wa Marekani au hata kujiondoa kabisa uanachama wa Nato (North Atlantic Treaty Organization). Huu ni umoja wa kijeshi unaoundwa na wanachama 32. Thelathini kutoka Ulaya na wawili (Canada na Marekani) kutoka Amerika ya Kaskazini.

Umoja huu uliundwa mwaka 1949 ukiwa na lengo la kuzisaidia nchi wanachama kiusalama, huku ukiongozwa na falsafa ya ikiwa mwanachama mmoja atashambuliwa, basi wanachama wote wataingilia kumtetea.

Faida za vichuguu katika uhifadhi

MCHWA ni jamii ya wadudu ambao huishi kwa kujenga viota ardhini, kwenye miti, kuta za nyumba na magogo ya miti. Mchwa ni wadudu ambao hawana asili ya ukali au vurugu endapo viumbe wamevamiwa na viumbe wengine kwenye makazi yao na hawawezi kupambana na wadudu wengine wakorofi kama sisimizi.

Wadudu hawa jamii ya mchwa husihi katika koo ambazo kitaalamu zinaitwa colonies. Koo za mchwa huchangia katika ukubwa wa kichuguu pia hutegemeana na idadi na aina ya mchwa.

Kwa mchwa wakubwa vichuguu huwa vikubwa na kwa mchwa wadogo vichuguu huwa vidogo. Vichuguu vya mchwa mara nyingi hupatikana hasa maeneo ya kitropic, yenye udongo aina ya mfinyanzi na kichanga isipokuwa maeneo yenye Calcium nyingi. Vichuguu hivi havifanani kwa muonekano wa rangi na maumbo.

Muundo wa vichuguu una matabaka mawili ambayo ni tabaka la udongo mgumu na tabaka na tabaka lenye matundu ya kupitishia hewa na kuwafanya mchwa kuwa imara na kupata hewa kwa urahisi.

Tafiti zinaonesha kuwa utengenezaji wa vichuguu kwa mchwa huanza kwa mchwa mmoja kutoa harufu (kemikali) na kuwavutia



mchwa wengine kudondosha udongo sehemu moja. Uwepo wa vichuguu vya mchwa katika eneo fulani ni moja ya kiashiria cha kibaolojia kuonesha kuwa ardhi ina rutuba ya kutosha.

Sambamba na hili, mchwa wanafahamika kisayansi kama mainjinia wa ikolojia (ecological engineer) kwani uwepo wao huboresha ardhi na kuifanya kuwa yenye rutuba.

Ujenzi wa vichuguu vya mchwa huanza kwa kukusanya na kusafirisha mabaki ya viumbe hai kama mimea na wanyama, pia punje ndogo za mbegu na udogo kwa kuchimba toka sehemu tofauti na kwenda kuweka sehemu moja (kwa mchwa wanaojenga vichuguu kwenye miti) ila kwa wanaojenga ardhini hutoa

udongo chini ya ardhi na kuuweka sehemu ya juu.

MUUNDO WA VICHUGUU

Muundo wa vichuguu au vijenzi hutofautiana kulingana na aina ya udongo na mabaki ya viumbe. Vichuguu ni kitovu cha rutuba katika ikolojia na hutofautiana kulingana na muda na nafasi (mahali) ambapo kichuguu hujengwa.

Vijenzi vya vichuguu hupatikana maeneo karibu na kiota au kichuguu kinapojengwa. Vitu muhimu ni kama vile mabaki ya mimea (majani), wanyama pia na udongo laini wa tabaka la chini ya ardhi. Asili ya vichuguu vina udongo wa mfinyazi ambao unawezesha kutunza maji na rutuba na kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Madini, Vitamini muhimu kwako hizi hapa



VITAMINI na madini yanafanya kazi ya kujenga kinga ya mwili, na yanapatikana katika mboga na matunda. Ni muhimu kwa makundi ya watu kama watoto, mama wajamzito, mama anaenyonyesha na wazee, kwani huzuia na kusaidia kupambana na maambukizi ya magonjwa.

Watu wengi hawali chakula cha kutosha chenye mboga na matunda, pamoja na vyakula vingine ambavyo ni vyanzo vya vitamini na madini. Hata hivyo, huwezi kula matunda au mboga kwa siku moja na kutarajia kutosheleza mahitaji ya mwili wako.

Kuongeza juisi za mboga kwa mlo wako, supu zenye virutubisho kama supuya mifupa, na ya mboga za majani zinaweza kusaidia sana kuuweka katika hali nzuri kiafya.

Yafuatayo ni makundi ya vitamini na madini yanayotumika kwa viwango vikubwa mwilini, na vyanzo vyake.

Vitamini C

Vitamini C inahitajika kwa ukuaji na ukarabati wa tishu katika sehemu zote za mwili pamoja na kuponya majeraha. Inasaidia mwili kuchukua na kutumia madini ya chuma, yaani Iron.

Vitamini C inapatikana kwa matunda jamii ya machungwa, ndimu, limau, pixie, paipai, mboga za majani ya kijani kibichi; spinach, brokoli, cauliflower, mboga za kienyeji, pia pilipili na strawberry. Mwili hauwezi kutengeneza vitamini C peke yake. Kwa hivyo, ni muhimu kula vyakula vingi vyenye Vitamini C kila siku.

Vitamini A

Vitamini A ni muhimu sana kwa ukuaji wa watoto, wamama wajawazito na pia watu wazima. Inasaidia kuunda na kudumisha meno yenye afya, tishu za mifupa, utando wa kamasi, na ngozi. Pia, huchangia kuona vizuri, haswa sehemu yenye mwanga mdogo.

Upungufu wa Vitamini A unaweza kusababisha shida za kiafya; ikiwa ni pamoja na

upofu ama kutoona vizuri, huongeza ukali na hatari ya maambukizo kama ugonjwa wa ukambi na kuhara, hatari ya upungufu wa damu na kifo kwa wanawake wajawazito na huathiri vibaya kijusi kwa kupunguza ukuaji.

Inapatikana katika mboga na matunda yaliyo na rangi ya njano na pia rangi ya machungwa kama vile karoti, viazi vitamu vyenye rangi ya machungwa, nyanya. Pia, maini, maziwa na mayai.

Vitamini D

Vitamini D husaidia mwili kuchukua kalsiamu na inaweka mifupa imara na katika mfumo wa neva, misuli, na kinga. Unaweza kupata vitamini D kupitia ngozi kutokana

na miale ya jua, na chakula kama uyoga, samaki, maziwa, mayai, maini na pia juisi ya machungwa.

Madini ya Kalsiamu

Kalsiamu inatumika kwa ujenzi wa mifupa na meno yenye nguvu. Pia ni muhimu kufanya misuli kusonga, moyo kupiga na mishipa ya damu kupanuka ili kusafirisha damu, na kutuma ujumbe kupitia mfumo wa neva.

Pata kalsiamu kutoka kwa maziwa, jibini, na vyakula vingine vya maziwa, na kutoka kwa mboga za kijani kibichi kama broccoli na bamia.

Madini ya chuma

Madini ya chuma inahusika na uzalishaji wa damu. Karibu asilimia 70 ya kiasi ya chuma mwilini hupatikana kwenye chembechembe nyekundu za damu na kwenye seli za misuli.

Chembechembe nyekundu za damu ni muhimu kwa kusafirisha Oksijeni katika damu kutoka kwenye mapafu hadi kwenye tishu za mwili. Bila Iron, huwezi kupata oksijeni ya kutosha kwa tishu zako.

Maeneo nyeti kwa uhifadhi wa ndege

NDEGE maji ni moja ya kundi muhimu sana la ndege katika uhifadhi, utalii na uchumi. Ndege wa maji au kama wanavyojulikana kwa kingereza waterbirds, ni ndege ambao mara nyingi hutegemea maji katika maisha yao.

Ndege hawa hupatikana zaidi maeneo yenye maji, kama vile kwenye maeneo ya ardhi oevu, mabwawa, maziwa, mito, chemichemi, bahari, au maeneo mengine yenye vyanzovya maji. Hutegemea maji kwa ajili ya kupata chakula, makazi, kuzaliana, au kupumzika.

Tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 10 ya spishi za ndege wote duniani wanategemea sana maji katika maisha yao. Hasa maeneo ya ardhi oevu au wetlands. Maeneo yenye maji yamekuwa na mchango mkubwa sana kwa uhifadhi wa ndege.

Mfano, Tanzania kuna ndege aina ya heroe (flamingo) ambao hupatikana katika ziwa Natroni, ndege hawa hutegemea ziwa hili lenye magadi kuzaliana. Mazingira na upekee wa ziwa Natroni umefanya kuwa sehemu muhimu sana duniani kwa uhifadhi, mazalia na makazi muhimu ya ndege hawa.

Hivyo majinisehemu muhimu sana ya maisha ya ndege

hawa, sehemu zenye ukame au uharibifu wa mazingira yao huwezi kuwakuta ndege maji, hivyo huwa kama kiashiria cha afya ya ikolojia ya mahali fulani.

Mfano, unaweza kuona aina fulani ya ndege maji wakiwa kando kando ya mito au maziwa au maeneo oevu. Mara nyingi utawakuta hapo wakijitafutia chakula chao na pia ni sehemu inayoendana na maisha wanayoishi.

Uoto unaoota kando ya vyanzo vya maji unakuwa na aina ya kipekee ya miti, misitu na hali ya hewa ambayo inawafaa ndege maji. Hata hivyo, ndegemaji husiadia kudumisha na kuendeleza ikolojia ya uoto ulioko kando ya maeneo yenye maji.

Endapo kutatokea uharibifu wa mazingira hayo, ndege hao wanaweza kutoweka kabisa katika eneo hilo. Mfano, kama kuna ndege maji wanaishi maeneo ya bwawa au mto, ikatokea mtu akaja kuharibu yale mazingira kwa kukata miti na kuyabadilisha kabisa mazingira hayo, ndege maji wanaweza kutoweka haraka sana.

Hata hivyo, maeneo mengi oevu, mabwawa na mito yanakabiliwa na hatari kubwa sana ya kuvamiwa na kutumiwa kwa shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, viwanda,

barabara au ujenzi wa mitambo mikubwa. Soma zaidi hapa; Zijue Faida Za Sensa ya Ndege wa Majini (Waterbirds)

Kwa kutambua hilo, hatuna budi kuangalia kwa makini miradi yetu ya maendeleo ambayo inafanyika au kupangwa kufanyika maeneo muhimu ya ndege maji. Kwasababu kuharibika kwa makazi yao ni jambo linaloweza kutokea haraka sana, lakini kurudisha kwa makazi yao ni jambo gumu, ambalo linachukua miaka mingi kurudi katika hali yake.

Tanzania ni nchi ya kipekee sana kwa uhifadhi wa ndege maji, uwepo wa mito mingi, mabwawa makubwa na madogo, maeneo makubwa ya ardhi oevu ambayo yana hadhi kubwa hadi kutambuliwa kama Ramsar site.

Mfano wa maeneo oevu yenye hadhi ya kimataifa hapa Tanzania ni kama ifuatavyo;

Malagarasi – Moyovozi, ilianzishwa mwaka 2000, ina ukubwa wa hekta 3,250,000. Ni eneo muhimu sana kwa uhifadhi wa ndege maji, mimea, ndege wanaohama, viboko, aina nyingi za samaki, na mamba, ni moja ya ardhi oevu kubwa barani Afrika.

Bonde la Kilombero, ni moja ya eneo kubwa la ardhi oevu, lina ukubwa wa hekta 796,735, ilianzishwa mwaka 2002, linatambuliwa kwa uwepo wa aina nyingi wa ndege wanaohama, idadi kubwa ya wanyama kama tembo, na mimea na samaki

Rufiji-Mafia-Kilwa, hili ni eneo muhimu sana la ardhi oevu, lina ukubwa wa hekta 596,906, lilianzishwa mwaka 2004. Eneo hili linahifadhi viumbe hai muhimu kama vile aina nyingi za mikoko, mwani, matumbawe, aina nyingi za ndege maji na aina nyingi za viumbe wa baharini.



Usiyoyajua kuhusu Twiga

TWIGA ni miongoni wa wanyamapori wa kipekee sana, upekee wao unawafanya wawe ni wanyama wanaovutia na wanaopendwa sana duninani. Hii inachangiwa na umbo lake kubwa na shingo ndefu kuliko wanyamapori wote.

Ni wanyama wanaopatikana barani Afrika pekee, ukienda Ulaya au mambara mengine wanafugwa kwenye bustani za wanyama. Twiga ni wanyama wanaotembea kwa madaha na maringo, hali ambayo inaongeza mvuto kwa watu wengi wanaomtazama.

Hata asili ya jina lake linahusishwa na namna anavyotembea kwa upekee, mfano, Waarabu walimuita "zaraf", wakimaanisha ni mnyama anayetembea haraka na kwa madaha au maringo.

Twiga kwa kingereza anaitwa 'Giraffe' na jina lake la kisayansi ni Giraffa camelopardalis. Ukiangalia hili neno camelopardalis. utaona kuna maneno mawili ambayo ni camel na pardalis, camel ni ngamia, na pardalis ni jina la kisayansi la chui, linaandikwa 'pardus' kwa Kilatini.

Hii ni kwasababu walimuona twiga ana umbo lenye mchanganyiko wa wanyama wawili, ambao ni ngamia na chui. Ukiangali vizuri utaona mwili wa twiga unakaribia kufanana na ngamia, lakini ngozi yake inafanana na chui.

Mpangilio wa madoa yaliyopo katika ngozi ya twiga haifanani na twiga mwingine. Unaweza kuwona twiga wengi sehemu moja, lakini wanatofautiana katika mpangilio wa madoa yao ya ngozi. Hawafanani kabisa.

Miguu ya mbele ni mirefu kuliko miguu ya nyuma, hivyo humsaidia kukimbia kwa haraka. Hata hivyo twiga dume ni mrefu na mkubwa zaidi



kuliko twiga jike. Dume ana urefu wa mita 5.3, jike mita 4.2.

Twiga jike anabeba mimba kwa siku 453-464, sawa na miezi 15. Mara nyingi huzaa mtoto mmoja, na mtoto jike akifikia miaka 3-4 anaweza kuchukua mimba, dume akifikisha miaka 4-7 anaweza kuzalisha jike.

Kuna aina au spishi 4 za twiga duniani. Tafiti za mwanzoni kabisa zilionyesha kuna spishi 9 za twiga. Lakini baada ya tafiti za kina za mazingira yao na kuchunguza kwa makini vinasaba vya kila spishi za twiga waligundua kuwa kuna spishi 4 tu za twiga na sio 9 kama ilivyokuwa mwanzoni.

Watafiti wa twiga, kama vile Shirika la Uhifadhi wa Twiga walifanya tafiti hizo na kubaini kuna aina 4 za twiga. Lakini pia shirika hili ambalo limejikita kufanya tafiti za kina kuhusu twiga, imesaidia sana sehemu nyingi Africa ambako kuna twiga.

Spishi 4 za twiga ni kama ifuatavyo; Twiga wa Kimasai, Masai (G. tippelskirchi), – Tanzania and Kenya -45,400

Twiga wa Kaskazini-Kusini mwa Chadi, Northern (G. Camelopardalis), CAR, DRC, W. Sudani-5900

Twiga wa Madoa ya Wavu, Reticulated (G. reticulata),

Ethiopia, Somalia and Kenya- 15,950

Twiga wa Kusini, Southern (G. giraffa)- Botswana, Namibia, Zimbabwe, Zambia, SA-49,850

Tanzania tuna Twiga wa Kimasai au Masai giraffe. Hii ni aina moja tu ya twiga iliyopo Tanzania. Lakini pia Tanzania ndio nchi yenye twiga wengi zaidi barani Afrika. Takwimu kutoka TAWIRI zinaonyesha tuna zaidi ya twiga 28,850.

Twiga ni mnyama wa taifa la Tanzania, ni mnyama anayeheshimika na kupendwa, ndio maana Serikali imezuia mnyama huyu kuwindwa.

Kutokana na upekee wa mnayama huyu, Serikali ya Tanzania iliamua kumfanya awe ni mnyama wa taifa. Utaona picha ya mnyama huyu ikitumika kama nembo kwenye maeneo mbali mbali. Mfano, kwenye fedha kuna nembo ya twiga, kwenye baadhi ya nyaraka za serikali kuna nembo ya twiga.

Wengi wanavutiwa na mnyama twiga na kuweka kama alama ya ufahari na mvuto. Ukienda kwa wale watu wanaochonga vinyago utaona nao wamechonga vinyago vingi vya wanyama mbali mbali, lakini huwezi kukosa kinyago cha twiga.



BURNA BOY HAKUNA BIFU

LAGOS, Nigeria
STAA wa Afrobeats, Seun Kuti, amejitoa katika bifu linaloendelea kati ya wasanii wawili, Burna Boy na Speed Darlington. Speed aliwahi kushikiliwa na polisi kwa kosa lake la kumdhalilisha Burna Boy baada ya mwenzake huyo kuhusishwa na P. Diddy. Sasa, akizungumzia bifu linaloendelea, Kuti alisema: "Nisingependa kuhusishwa na bifu lao. Sisemi kwamba niko upande wa Burna Boy kwa kuwa alinipa dhahabu."

CHIOMA KUMBE MTUPU

LAGOS, Nigeria
MWIGIZAJI wa kike anayefanya vizuri katika soko la filamu la Nigeria, Chioma Akpotha, amekanusha taarifa zilizodai kuwa amejifungua. Ripoti zilizodai amepata mtoto wa kiume zilivuma mitandaoni na kusababisha rafiki yake,

Omoni Oboli, amtumie ujumbe wa pongezi. Hata hivyo, akijibu ripoti hizo, Chioma alisema mtoto pekee aliye naye kwa sasa ni chaneli yake mpya ya YouTube.



DRAKE MWAMBA WAO

LOS ANGELES, Marekani
SUPASTAA wa Hip hop, Drake, ametajwa na jarida la Billboard kuwa ndiye rapa bora wa karne hii ya 21. Katika ripoti hiyo ya hivi karibuni, Nick Minaj amekuwa rapa pekee wa kike kuingia, huku mpinzani wa Drake, Kendrick Lamar, akishika nafasi ya nane. Nafasi ya pili imekwenda kwa mkongwe wa muziki huo wa 'kufokafoka', Eminem, akifuatiwa na Kanye West, Nelly na Jay-Z.

GUARDIOLA AJIPANGA

MANCHESTER, England
KOCHA wa Manchester City Pep Guardiola anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Uingereza Jack Grealish, 29, huku kukiwa na mipango ya kukimarisha kikosi cha City. Inter Milan wanaibuka wapinzani wakuu wa Liverpool katika mbio za kumsajili kiungo wa Ujerumani Joshua Kimmich huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akiingia akisalia na miezi michache katika mkataba wake na Bayern Munich.



LIVERPOOL YAITWA KWA PEDRO


LONDON, England
MSHAMBULIAJI wa Brighton wa Brazil Joao Pedro, 23, anataka kujiunga na Liverpool majira ya joto. Naye straiika wa wa Canada Jonathan Davidyuko tayari kuondoka katika klabu hiyo kama mchezaji huru msimu huu wa joto.

WHARTON JICHO LA REAL MADRID

MADRID, Hispania
WASAKA vipaji wa Real Madrid wamekuwa wakimfuatilia kiungo wa England Adam Wharton tangu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 arejee kwenye kikosi cha kwanza cha klabu ya Crystal Palace. Nayo Liverpool wameanza mazungumzo na Conor Bradley kuhusu kandarasi mpya ya miaka mitano ambayo itamuwezesha beki huyo wa Ireland Kaskazini, 21, kupata nyongeza ya 650%.

BART KUJIKUTA CHELSEA?

LONDON, England
CHELSEA inamfuatilia kwa karibu kipa wa Uholanzi na klabu ya Brighton Bart Verbruggen, 22, kwa ajili ya uhamisho wa majira ya joto. Nazo Manchester United, Tottenham na Arsenal zimeonyesha nia ya kumsajili Benjamin Sesko kutoka RB Leipzig na mshambuliaji huyo wa Slovenia mwenye umri wa miaka 21 ana kipengele cha kutolewa ambacho kinaweza kutumika msimu huu wa joto.



JOHAN VASQUEZ MTU KATI

LONDON, England
TIMU za Brentford na Fulham zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa Mexico Johan Vasquez, 26, kutoka Genoa. Fulham na Sporting wanamuwinda beki wa Ugiriki, Georgios Vagiannidis, huku Sporting wakiwasilisha dau la euro 10m (£8.3m) kwa Panathinaikos.



CHAMA MTAMU!

**>>KAMA UNAOGOPA
KUMSIFIA SHAURI YAKO,
ILA NDO' UKWELI**

NA MWANDISHI WETU

ERASTO Nyoni kiraka anayetimiza majukumu yake ndani ya kikosi cha Namungo kinachonolewa na Kocha Mkuu, Juma Mgunda ameweka wazi kuwa nyota Clatous Chama amebadilika hasa kwenye upande wa spidi ila watu wanamtazama kwa mazoea.

Ipowazikwamba Chama nimchezaji wa kwanza kutambulishwa ndani ya kikosi cha Yanga kwenye dirisha kubwa la usajili ilikuwa ni Julai Mosi 2024 ambapo aliibuka hapo akiwa ni mchezaji huru baada ya kumaliza kandarasi yake ndani ya kikosi cha Simba.

Chama alipokuwa Simba alikuwa chaguo la kwanza lakini kwa sasa ndani ya kikosi cha Yanga ambacho kwenye anga la kimataifa kimegotea hatua ya makundi sio chaguo la kwanza amekuwa akipokezana namba na Aziz Ki ambaye naye ni kiungo mshambuliaji wakati mwingine Pacome.


Nyoni aliwahi kucheza na Chama katika kikosi cha Simba kabla ya kukutana na Thank You na

sasa anaendelea kutimiza majukumu ndani ya Namungo ambayo Februari 27 2025 ilishuhudia ubao wa Uwanja wa Azam Complex ukisoma Azam FC 1-1 Namungo.

Kiungo huyo amesema: "Chama amebadilika kwenye suala zima la uchezaji ila kwa kuwa yupo kwenye timu mpya watu wanamuangalia kwa mazoea tu ninaweza kusema hivyo. Ukimuangalia kwenye uchezaji wake ameongezeka

spidi lakini kuna watu hawawezi kujua.

"Ninaweza kusema ni kumzoea si unamuona namna anavyocheza. Watu wamemzoea Chama lakini hawataki kumuona anachezaji kule kuna wachezaji ambao ni wazuri hivyo ushindani utakuwa mkubwa, lakini hapana amebadilika uchezaji mwangalie kwenye mechi zote amebadilika amekuwa kwenye spidi."



KOMBE LA SHIRIKISHO KUNOGA

NA MWANDISHI WETU

WENYEJI, JKT Tanzania juzi walifanikiwa kutinga Hatua ya 16 Bora Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), michuano inayodhaminiwa na Benki ya CRDB baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Biashara United ya Mara Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mweni Jijini Dar es Salaam.

Mabao ya JKT Tanzania yalifungwa na Shiza Kichuya dakika ya 19 na Najim Magulu dakika ya 47, wakati bao pekee la Biashara United lilifungwa na Freddy Kiwale dakika ya 82.

Nayo Tabora United ikaitupa nje Transit Camp kwa penalti 4-2 kufuatia sare ya kufungana bao 1-1 Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Mabingwa wa zamani wa michuano

hiyo, Mtibwa Sugar wakaitupa nje Town Stars kwa kuichapa mabao 5-3 Uwanja w Manungu Complex, Morogoro.

Mechi nyingine za Hatua ya 32 Bora, Mbeya Kwanza iliichapa Mambali Ushirikiano mabao 3-0 Uwanja wa Nangwanda Sijaona mjini Mtwara.

Nao Songea United wakapata ushindi wa 1-0 ugenini dhidi ya Polisi Tanzania Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati Giraffe Academy waliilaz Green Warriors 1-0 Uwanja wa Uwanja wa Azimio mjini Katavi.